

Makosa ya Kiuandishi katika Kamusi za Kiswahili na Athari zake kwa Watumiaji

*Jacob Haule*¹

Chuo Kishiriki cha Elimu Mkwawa
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

na

*Titus Mpemba*²

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

DOI: <https://doi.org/10.56279/mulika.na43t1.3>

Ikisiri

Lugha huenea na kuimarika kupitia kuandaa maandishi ya kusomwa na watu wengi duniani na ujumbe wa kimaandishi humfikia vizuri msomaji iwapo utaandikwa vizuri. Mbali na kufikisha ujumbe, uandishi mzuri pia huvuta makini ya msomaji ilhali uandishi mbaya humkanganya na kumchusha. Kwa kuwa kamusi hukusudiwa kuwa miongozo ya usanifu na ufasaha wa lugha husika, inatarajiwa kuwa zinaepuka makosa ya kiuandishi. Kwa kutumia Nadharia ya Urafiki wa Kamusi kwa Mtumiaji, makala haya yanahakiki kiwango cha uzingativu wa kaida ya uandishi mzuri katika kamusi za Kiswahili, yakilenga Kamusi Kuu ya Kiswahili (KKK), Kamusi ya Kiswahili Sanifu (KKS) na Kamusi la Kiswahili Fasaha (KKF). Ili kulifikia lengo hili, waandishi walijihusisha na kubainisha makosa ya kiuandishi tu na kujadili athari zake kwa wasomaji. Data zilikusanywa kupitia uchambuzi matini. Matokeo yanaonesha kuwa kamusi madhukura zina makosa ya udondoshaji na uchopekaji, matumizi muhali ya njeo, uradidi, unafasishaji usio sahihi, na upatanishi potofu wa kisarufi, ambayo ama huwakosesha watumia kamusi maana sahihi au huwachusha. Kutokana na matokeo haya, waandaaji na wachapishaji wa kamusi wanashauriwa kuweka jitihada za kuyaepuka makosa ya aina hii. Hili litahakikisha kuwa ujumbe wa kamusi unawafikia watumiaji kama ulivyokusudiwa na kuwaepushia athari zilizotajwa.

1.0 Utangulizi

Kamusi za lugha hujumuisha taarifa mbalimbali za kifonetiki, kifonolojia, kimofolojia, kisintaksia na kisemantiki (Mdee, 2010; Matinde, 2012). Taarifa hizo humwezesha mtumiaji wa kamusi kutimiza malengo yake kadiri ya mahitaji yake. Kutokana na kusheheni taarifa mbalimbali za lugha, kamusi ni maandiko muhimu sana katika kuhifadhi lugha, kutoa miongozo ya matumizi sahihi ya lugha na kujenga misingi ya

¹ Barua pepe: haulejacob@yahoo.com

² Barua pepe: titus.mpemba@udsm.ac.tz

mustakabali madhubuti wa maendeleo ya lugha. Licha ya kamusi kuwa na umuhimu huu, kuna nyakati ambapo huwasababishia watumiaji wake changamoto kutokana na kuwa na makosa au udhaifu mwingine wa aina mbalimbali. Makala haya yanachunguza na kuhakiki ujitokezaji wa makosa ya kiuandishi katika kamusi za Kiswahili, ikilenga KKK, KKS na KKF kama kamusi kuu zinazoaminiwa kwa watumiaji wengi kutokana na kuandaliwa na taasisi zilizokasimishwa mamlaka ya kustawisha na kuendeleza Kiswahili ndani na nje ya Tanzania. Kadhalika, makala yanachunguza na kutathmini athari za makosa ya kiuandishi katika kamusi tajwa kwa watumiaji.

Uchunguzi na uhakiki madhukura ni muhimu kufanyika kwa sababu husaidia kuibuliwa kwa changamoto mbalimbali katika kamusi (Mwenda, 2016) na kupendekezwa kwa namna ya kuzikabili. Suala hili huwafanya wanaleksikografia watunge kamusi mpya au wadurusu kamusi zilizopo ili kupata matoleo bora zaidi yanayokidhi mahitaji ya watumiaji wa lugha husika (Wiegand, 1983; Hartmann, 2001). Kwa hiyo, maarifa ya makala haya yatawanufaisha wanaleksikografia, ambao ni waandaaji wa kamusi, pamoja na wachapishaji, hususani wa kamusi teule. Kupitia makala haya, wanaleksikografia na wachapishaji watapata fursa ya kutambua makosa waliyoyafanya katika kamusi husika, na hivyo, kuyatumia maarifa hayo katika kufanya udurusu wa kamusi husika kwa kuyarekebisha makosa yaliyopo wakati wa kuandaa matoleo yajayo ya kamusi yatakayokuwa bora zaidi. Kadhalika, maarifa ya makala haya yatawanufaisha watumiaji wa lugha kwa ujumla kwa kutambua kuwa wanapaswa kuchukua hadhari watumiapo kamusi kwa kuwa makosa kadhaa yanaweza kujitokeza. Kwa ujumla, matokeo ya utafiti huu yanatoa mchango katika maendeleo ya lugha ya Kiswahili. Wajifunzaji wa Kiswahili kutoka mataifa mbalimbali hutumia kamusi kama rejea zao kuu za ujifunzaji na huwa hawajui kipi ni sahihi wala kipi si sahihi; kwao, kila kilichomo kamusini ni sahihi. Hivyo, makosa haya yakisahihishwa kutokana na uzingatiwaji wa matokeo ya utafiti huu, kamusi zitakuwa na Kiswahili sanifu kisichokuwa na makosa ambacho tutaweza kukieneza vyema.

Makala yana sehemu tano. Sehemu ya kwanza ni utangulizi unaodokeza mwenendo wa makala na umuhimu wa utafiti ili kumpatia msomaji ramani na uhalali wa makala. Sehemu ya pili inafafanua dhana za msingi zilizotumika katika makala ili kuwapatia wasomaji uelewa wa namna moja na uliokusudiwa na waandishi. Kadhalika, sehemu hii inatoa maelezo mafupi kuhusiana na tafiti tangulizi zilizohakiki kamusi. Lengo ni kuuweka utafiti huu katika muktadha mwafaka na kubainisha pengo la kiutafiti. Sehemu ya tatu inaelezea mwega wa kinadharia, umuhimu wa utafiti na jinsi data zilivyopatikana. Sehemu ya nne inawasilisha na kujadili matokeo ya utafiti na sehemu ya mwisho ni hitimisho. Baada ya matini kuu ya makala, kuna orodha ya marejeleo yaliyotumika.

2.0 Dhana za Msingi na Mwelekeo wa Uchunguzi wa Makosa ya Kiuandishi katika Kamusi

Kwa kuwa istilahi hubeba dhana mbalimbali, inafaa kubainisha dhana zinazobebwa na istilahi muhimu zilizotumika katika makala haya ili kuwa na uelewa wa pamoja. Dhana hizo ni ‘makosa ya kiuandishi’, ‘kamusi’, na ‘uhakiki wa kamusi’ kama zinavyotumika katika makala haya. Dhana ya makosa ya kiuandishi inatumika katika makala haya kwa maana ya dosari zinazojitokeza kutokana na mwandishi kukiuka taratibu za kiuandishi au za kisarufi ambazo hukwaza uwasilishaji wa ujumbe uliokusudiwa au huleta tu maudhi kwa msomaji na kumfanya amwone mwandishi kama mtu asiye makini na asiyeipenda wala kuijali kazi yake (King’ei, 2014; Mpemba, 2018; Widyaningsih, 2018). Fasili hii inasisitiza umuhimu wa kuwa na maandishi bora yanayowasaidia watumiaji badala ya kuwakanganya na kuwaudhi. Kuhusiana na dhana ya kamusi, wanaleksikografia wengi wanakubaliana kuwa ni kitabu chenye orodha ya maneno yaliyopangwa kwa utaratibu maalumu kama vile kufuata alfabeti na kutolewa fasili na taarifa mbalimbali, ikiwa ni pamoja na tahajia, silabi, matamshi, mifano ya matumizi, etimolojia, maana za vidahizo, na taarifa za kisarufi kama vile kategoria, maumbo ya wingi na umoja, ngeli, na uhusika wa vitenzi (Hartmann, 1983; Jackson, 2002; Mdee, 2010; TUKI, 2019). Fasili hii ndiyo inayotumika pia katika makala haya kwa kuwa inafumbata takribani vipengele vyote muhimu vinavyozingatiwa katika kamusi.

Uhakiki wa kamusi unaelezwa kuwa ni mchakato wa kuchambua au kutathmini ubora na udhaifu wa kamusi zilizopo kwa lengo la kupima kufaa kwake kimatumizi (Wiegand, 1983; Hartmann, 2001). Tathmini hiyo huweza kuabiri taarifa mbalimbali za kileksikografia katika kamusi na inaweza kuwa ya matini ya kamusi, mawanda ya kamusi, uhalali wa kamusi au matumizi ya kamusi. Katika makala haya, uhakiki unaofanywa ni wa matini ya kamusi kwa kuzingatia namna vidahizo vilivyoingizwa na vilivyofasiliwa (Jackson, 1996). Uingizaji na ufasili wa vidahizo huwa na athari kubwa katika kamusi kwa kuwa watumiaji wengi wa kamusi hutafuta zaidi maana za vidahizo (Hans, 2012). Hivyo, kukiwa na makosa ya kiuandishi katika fasili za vidahizo kama vile hitilafu ya njeo, upatanisho muhali wa kisarufi, matumizi fyongo ya vihusishi, wingi na umoja, na viunganishi; kuna uwezekano wa mtumiaji kutopata vyema maana za vidahizo husika. Ndiyo maana, makala haya yamejielekeza katika uhakiki wa matini ya kamusi ikibainisha makosa ya kiuandishi katika kamusi teule na hali kadhalika kutoa mapendekezo.

Utafiti huu si wa pekee wala wa kwanza kuhakiki kamusi kwa kuwa unachota maarifa kutoka tafiti zilizotangulia. Mdee (2004) anaziaua tafiti hizo kwa ufupi lakini kwa utoshelevu. Anasema kuwa katika historia ya muda mrefu, kamusi daima zimekuwa zikihakikiwa, jambo ambalo limesaidia maendeleo yake kuanzia hatua ya faharasa hadi

kuwa vitabu vyenye taarifa nyingi za lugha na tamaduni mbalimbali. Anawataja baadhi ya wahakiki wa awali kabisa wa karne ya 18, aghalabu bila kuonesha miaka ya kazi zao, kuwa ni pamoja na Addison ambaye alipendekeza kuwa kamusi ya Kiingereza iwe na madondoo kutoka maandikoni. Wengine anaowataja ni Swift, Defoe na Pope, ambao walipendekeza kuwa kamusi iawe na kutunza kumbukumbu za lugha ya Kiingereza. Mapendekezo hayo yalitiliwa maanani na Johnson (1755). Hata hivyo, naye alikumbana na uhakiki wa Richardson na Trench kwa kutozingatia kanuni za leksikografia. Maoni ya wahakiki hao yalisaidia kuboreshwa kwa kamusi kwani James Murray na wanaleksikografia wengine walikonganya kamusi ya Kiingereza ya *Oxford English Dictionary* wakizingatia kanuni hizo. Mdee pia anataja wahakiki wa karne ya 20, wakiwamo Lemmens na Wekker (1986), ambao walihakiki sarufi katika kamusi za wanafunzi wa Kiingereza na kubainisha dosari na kukosekana kwa urari katika uingizaji wa taarifa za kisarufi kwenye kamusi hizo. Utafiti wa Mdee ni muhimu sana katika kujua historia na maendeleo ya uhakiki wa kamusi. Hata hivyo, umeangazia uhakiki wa kamusi za Kiingereza tu.

Tafiti zinazohakiki kamusi za Kiswahili ni chache na zimejikita zaidi katika kamusi za Kiswahili-Kiingereza au Kiingereza-Kiswahili. Kwa mfano, Mdee (2004) anahakiki kamusi ya Kiingereza-Kiswahili ya Kirkeby (2000) kwa kutalii vipengele vya wingi wa taarifa, ubora wa taarifa, na usasa wa kamusi. Chuwa (1996) alichunguza matatizo mbalimbali ya kamusi za Kiswahili kuanzia mwanzo wa historia ya leksikografia ya Kiswahili, huku akijielekeza zaidi katika *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (TUKI, 1981). Anabainisha matatizo kama vile uteuzi mbaya wa msamiati, kuwa na sinonimu na homonimu nyingi, kamusi kukosa malengo maalumu, na kuwa na vidahizo vichache. Kwa ujumla, tafiti zilizopo, kadiri ya uelewa wa maandishi wa makala haya, hazimakinikii makosa ya kiuandishi. Hivyo, utafiti huu unajaribu kuziba pengo hilo.

3.0 Mwega wa Kinadharia, Mawanda ya Utafiti, na Mbinu ya Ukusanyaji wa Data

Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Urafiki wa Kamusi kwa Mtumiaji iliyoasisiwa na Prinsloo na Gouws (1996). Nadharia hii inasema kwamba kamusi ni lazima iwe rafiki kwa watumiaji kwa kuzingatia urahisi wa kutumia na kukidhi mahitaji yao. Hivyo, kamusi ikiwa na makosa ya kiuandishi yanayokwaza kueleweka kwa maana ya kidahizo au kusababisha maudhi kwa watumiaji, inakiuka kanuni hii na, hivyo, si rafiki kwao. Kamusi nzuri haioneshi tu ushughulikiaji mzuri wa lugha kuhusiana na uteuzi maalumu wa vipashio vya kileksika, bali pia humpatia mtumiaji taarifa anayoitaka au anayoitafuta (Haas, 1962). Kwa sababu hii, urafiki wa kamusi kwa mtumiaji, mtazamo ambao umekuwa maarufu siku hizi katika metaleksikografia, huwataka wanaleksikografia waandae kamusi zao kulingana na ujuzi wa kiutafiti, kwa kuzingatia

makundi ya lugha lengwa yaliyobainishwa kinaganaga na kwa kuzingatia mahitaji ya watumiaji wanaolengwa na kamusi.

Kwa kuwa uhakiki wa kamusi unaweza kuelekezwa katika vipengele anuwai kama vile mawanda ya kamusi, matini ya kamusi, uhalali wa kamusi, na matumizi ya kamusi, makala haya yasingeweza kuchunguza vipengele vyote. Hivyo, yalikusika na uhakiki wa matini kwa sababu matini ndiyo huwalenga watumiaji moja kwa moja. Uhakiki wa matini ya kamusi hushughulikia uingizaji wa msamiati pamoja na fasili za vidahizo (Wiegand, 1983; Jackson, 1996). Kwa hiyo, makala haya yanatathmini vipengele hivi huku yakimakinika zaidi na kipengele cha fasili za vidahizo kwa kuwa watumiaji wengi wa kamusi aghalabu hutafuta taarifa hii katika kamusi.

Ingawa kamusi za Kiswahili ni nyingi, kama ilivyokwisha dokeza awali, utafiti huu ulijikita katika kamusi tatu tu, ambazo watafiti waliona kwamba ndizo zinazoaminiwa zaidi na watumiaji kutokana na kuandaliwa na taasisi zilizokasimishwa mamlaka ya kustawisha na kuendeleza Kiswahili. Kama zilivyokwisha dokeza, kamusi hizo ni KKK, KKF, na KKS. KKK ni kamusi iliyoandaliwa na BAKITA na kuchapishwa na Longhorn kwa mara ya kwanza mnamo mwaka 2015 ikiwa na lengo la kumsaidia msomaji kujua na kuainisha kwa usahihi msamiati wa Kiswahili kimuundo, kimatamshi na kimatumizi. Kamusi hii, ambayo kwa sasa toleo lililopo ni la tatu, ni muhimu kwa watu wote: wanaojifunza na wanaotaka kutumia Kiswahili safi, sanifu, fasaha na kamilifu (BAKITA, 2022). Hii ni kamusi ya lugha yenye vidahizo vingi na vipya. Kuhusu KKF, imeandaliwa na kuchapishwa BAKIZA mnamo mwaka 2010 kwa lengo la kuendeleza Kiswahili na utamaduni wa Mswahili, kuwaongoza watumiaji wa lugha kuhusiana na matumizi fasaha ya Kiswahili sambamba na kuwa rejea ya msamiati na matumizi halisi ya maneno ya Kiswahili (BAKIZA, 2010).

Ikumbukwe kuwa BAKITA na BAKIZA yote ni mabaraza yenye mamlaka ya kisheria ya kukuza na kueneza Kiswahili, moja kwa Tanzania Bara na moja kwa Zanzibar. Kwa upande wa KKS, yenyewe imeandaliwa na Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI), sasa ikijulikana kama Taasisi ya Taaluma za Kiswahili (TATAKI) na kuchapishwa kwa mara ya kwanza na Oxford University Press mnamo mwaka 1981. Hivi sasa toleo lililopo ni la nne. Jukumu mojawapo la taasisi hii ni kulinda usanifu wa Kiswahili. Jambo hili hutekelezwa kwa kuandaa kamusi inayosimamia matumizi ya Kiswahili sanifu. KKS imeandaliwa ili kukidhi haja ya kimatumizi kwa ujumla. Kutokana na umuhimu wa kamusi hizi, watafiti waliona ni vyema kufanya tathmini ya makosa ya kiuandishi katika kamusi hizo ili kusaidia katika mchakato wa kupata kamusi bora zaidi katika matoleo yajayo kwa manufaa ya umma mpana wa watumiaji.

Mbinu ya uchambuzi matini ilitumika katika ukusanyaji wa data kutoka katika kamusi teule. Katika mbinu hii, mtafiti husoma kwa makini na kwa weledi maandiko maktabani kwa kuwa yanaweza kuwa chanzo cha data anazozihitaji (Kombo na Tromp, 2006). Kwa kuzingatia maelezo haya ya Kombo na Tromp, fasili zote za vidahizo vya kamusi teule zilisomwa na watafiti kwa makini na kwa weledi ili kuhakikisha kwamba hawaishii kufikia mahitimisho yanayotokana na majumuisho ya kiusampulishaji tu.

4.0 Makosa ya Kiuandishi katika KKK, KKS na KKF

Kwa kutumia mbinu ya utafiti iliyofafanuliwa katika sehemu iliyotangulia, watafiti walibaini makosa mbalimbali ya kiuandishi ambayo ni vyema yakawekwa bayana ili kuwasaidia waandaaji na wachapishaji wa kamusi husika wayashughulikie kwa ajili ya kuboresha matoleo yajayo pamoja na kuwasaidia watumiaji wa kamusi hizo kwa ujumla waweze kupata kamusi ambazo ni rafiki kwao. Makosa hayo yanawasilishwa katika vipengele vinavyofuata.

4.1 Makosa ya Uradidi Usio na Sababu

Uradidi ni utaratibu utumikao katika kuunda maneno mapya au kuweka msisitizo fulani kwa kurudia sehemu ya neno au neno zima (Rubanza, 1996; Matinde, 2012). Kama tutakavyoeleza baadaye, uradidi huwa na dhima maalumu pale unapotumiwa na mwandishi kwa kukusudia. Hata hivyo, data zilizokusanywa kutoka kamusi teule zinaonesha kwamba kuna maneno katika kamusi hizo ambayo yamerudiwarudiwa katika fasili mbalimbali bila sababu maalumu. Majedwali namba 1 na 2 yanabainisha mifano ya makosa hayo.

Jedwali Na. 1: Makosa ya Uradidi Usio na Sababu katika KKF

Kidahizo	Fasili
kachumbari	mchanganyiko wa vitunguu, tungule, limau au ndimu au siki, chumvi na pilipili.

Chanzo: BAKIZA (2010)

Jedwali Na. 2: Makosa ya Uradidi Usio na Sababu katika KKS

Kidahizo	Fasili
chokonoa	toa kitu kutoka mahali fulani kwa taabu

Chanzo: TUKI (2019)

Data katika Jedwali Na. 1 na Jedwali Na. 2 zinaonesha uradidi usio na sababu. Katika Jedwali Na. 1, kuna fasili za vidahizo zenye maneno yaliyoradidiwa kimakosa. Mathalani, kuna uradidi wa neno **au** katika fasili ya *kachumbari* ambao ungeondolewa kwa kutumia alama ya mkato tu. Kadhalika, katika Jedwali Na. 2, mwandishi

hakupaswa kurudia neno **kutoka**, kwa sababu mtu anapotoa kitu, ni dhahiri kwamba kitatoka.

Urudiarudiaji wa maneno usio na sababu maalumu, kama unavyoonekana katika data, unamkanganya msomaji na kumpa usumbufu wakati wa kusoma. Hivyo, ni kosa katika maandishi ya matini yoyote kwa kuwa uradidi unapaswa kufanyika pale tu kunapokuwa na sababu maalumu. Suala hili pia limefafanuliwa na wataalamu mbalimbali. MATHALANI, GENC na WENZIE (2010) wanaeleza kuwa dhima kuu ya uradidi ni kuwezesha mawasiliano na kwamba ni mbinu ambayo hutumiwa sana na wazungumzaji wa lugha mbalimbali ulimwenguni. Kadhalika, jambo hili limeelezwa na RUBANZA (2006) kwamba hujitokeza katika sehemu ya neno au neno zima kwa lengo la kutilia mkazo jambo au kuonesha kuwa jambo hilo hutokea mara kwa mara. AKIFAFANUA dhima za uradidi, MNENUKA (2010) anasema kuwa uradidi unaweza kutumika katika kudhoofisha, kuimarisha, kuongeza na kupunguza msisitizo wa dhana husika. Hata hivyo, uradidi unaojitokeza katika kamusi teule hauna malengo ya kuunda maneno wala kuweka msisitizo, bali ni makosa ya kiuandishi yanayofanya fasili za vidahizo husika zisilete maana iliyokusudiwa na zipoteze mantiki au zimkere tu msomaji. Kamusi zenye makosa yanayomkanganya mtumiaji zinakosa sifa ya urafiki inayohimizwa na Nadharia ya Urafiki wa Kamusi kwa Watumiaji.

4.2 Makosa ya Kitahajia

Makosa ya kitahajia ni yale yanayohusiana na masuala ya uandikaji wa herufi zinazounda neno fulani ambalo ni kubalifu (WANYENYA, 2015). Makosa ya aina hii yaliyojitokeza katika kamusi teule ni kama vile udondoshaji, uongezaji na ubadalishaji na yanawasilishwa katika vipengele vinavyofuata.

4.2.1 Makosa ya Udondoshaji

Udondoshaji ni utaratibu wa kuondoa kipashio kimojawapo cha kiisimu katika silabi, neno, kirai au sentensi (BAKITA, 2022). Katika utafiti huu, tumebaini kuwapo kwa udondoshaji wa herufi, maneno na vifungu vya maneno katika fasili za vidahizo ambao unasababisha vipashio kama herufi, silabi, maneno au vifungu vya maneno vya viambajengo lengwa visitimie. Kutotimia kwa vipashio katika viambajengo vinavyohusika kunasababisha kutokamilika kwa viambajengo husika, jambo linalosababisha viambajengo hivyo kutokuwa sahihi. Kutokana na hali hiyo, udondoshaji huo unaleta vikwazo katika uelewekaji wa fasili husika kama inavyooneshwa na data katika majedwali namba 3 hadi 5.

Jedwali Na. 3: Makosa ya Udondoshaji katika KKK

Kidahizo	Fasili
rupia	sarafu ya asili ya Kihindi iliyokuwa ikitumika kwenye himaya ya kikoloni ya zamani ya Afrika Mashriki
agizo	<i>ch.</i> tamko rasmi la mtu au chombo chenye mamlaka kuhusu utekelezji wa jambo
kadhi	<i>b.</i> mtu anayesema sheria za Kislamu aliyepewa mamlaka ya kisheria ya kusimamia na kutoa uamuzi wa masuala ya ndoa na mirathi na kutatua migogoro yote inayohusiana na dini ya Kiislamu.
Kiwolfu	lugha ya kiafrika iliyokuwa na hati zake yenyewe inayotumika (Afrika Magharibi)

Chanzo: BAKITA (2022)

Jedwali Na. 4: Makosa ya Udondoshaji katika KKF

Kidahizo	Fasili
maasi	vitendo visivyokubalika kwa mujibu wa maarisho ya Mwenyezi Mungu
mangrini	sehemu inayofngwa kamba ya nanda ili kukifanya chombo kiwe karibu na nanga.
kete	mbegu ngumu yenye ung aavu na rangi ya kijivujivu inapokauka; komwe. Kitu chochote k.v. kijiwe au kaure kinachotumiwa katika mchezo wa bao la vishimo.

Chanzo: BAKIZA (2010)

Jedwali Na. 5: Makosa ya Udondoshaji katika KKS

Kidahizo	Fasili
karakara	tunda la mkarara lenye nyama za nyuzinyuzi na mbegu nyingi nyeusi kwa ndani ambalo hutumika kutengezea sharubati
kaukau²	chakula kilichotengenezwa kwa k.v. viazi vilivyokatwakatwa vyembamba na kuchomwa katika mafuta hadi vikakauka

Chanzo: TUKI (2019)

Data zinazoonekana katika majedwali namba 3 hadi 5 zinadhihirisha namna udondoshaji ulivyojitokeza. Udondoshaji huo ni wa aina mbili. Kwanza, kuna udondoshaji wa baadhi tu ya herufi au silabi katika neno. Huu umejitokeza katika Jedwali Na. 3 ambapo fasili ya kidahizo *kadhi* ina neno **Kislamu**. Katika neno hili, irabu *i* ilipaswa kuwapo kati ya kiambishi ngeli **Ki-** na mzizi **-islamu** ili kupata neno sahihi *Kiislamu*. Aidha, katika fasili ya kidahizo *rupia*, neno **Mashriki** limefanyiwa udondoshaji. Neno hili lilipaswa kuwa na irabu *a* kati ya **Mash-** na **-riki** ili kupata neno kubalifu *Mashariki*. Vilevile, neno **utekelezji** katika kidahizo *agizo* limedondosha irabu *a* iliyotakiwa kuwa kati ya **utekelez-** na **-ji** ili kupata neno la Kiswahili

utekelezaji. Kadhalika, katika kidahizo **Kiwolfu**, kidahizo chenyewe kimedondosha herufi **-o-** baina ya **-l-** na **-f-** kwa sababu lugha inayofafanuliwa hujulikana kama **Kiwolofu**. Jambo hili limejitokeza pia katika KKF kama inavyooneshwa na data iliyo katika Jedwali Na. 4 ambapo kuna udondoshaji wa herufi **-m-** katika neno **maarisho** la kidahizo *maasi*. Neno sahihi linapaswa kuwa *maamrisho*. Pia, katika kidahizo *mangrini*, neno **inayofngwa** limefanyiwa udondoshaji wa herufi **-u-** ambapo neno sahihi lilipaswa kuwa *inayofungwa*. Katika KKS, kama tunavyoweza kuona katika Jedwali Na. 5 kwenye fasili ya kidahizo *karakara*, neno **mkarara** limedondosha silabi **-ka-** ambayo ilipaswa kuwa silabi ya pili kutoka mwisho. Aina ya pili ya udondoshaji ni udondoshaji wa neno zima au kifungu cha maneno kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 5. Katika jedwali hili, kifungu cha maneno **na kuwa vipande** kimedondoshwa kabla ya neno **vyembamba** katika fasili ya kidahizo *kaukau*². Pia, katika kidahizo *kete*, kuna udondoshaji wa alama ya king`ong`o (`) katika neno ambalo limeandikwa **ung aavu** badala ya **ung`aavu**.

Matokeo ya utafiti huu kuhusiana na udondoshaji yanajazia pengo la utafiti katika tafiti zilizotangulia. Mathalani, Lupogo (2020) analishughulikia tatizo hili lakini anajielekeza katika udondoshaji wa sauti/herufi ‘h’ pekee. Kwa mujibu wa Ontieri (2022), udondoshaji ni hali ya kuondoa kipashio katika neno kwa namna ambayo inakiuka taratibu za lugha husika na, hivyo, huathiri maana ya tungo. Tofauti na utafiti huu, utafiti wa Ontieri ulijikita katika athari za lugha ya kwanza katika lugha ya pili.

4.2.2 Makosa ya Uongezaji wa Sauti, Silabi au Kifungu cha Maneno

Kwa mujibu wa TUKI (2019), kuongeza ni kuweka zaidi. Hivyo, katika makala haya, uongezaji unatumika kwa maana ya uwekaji wa vipashio vya ziada katika viambajengo vinavyolengwa. Data zilizopatikana katika kamusi teule zinabainisha kuwa kuna viambajengo vilivyotumika katika fasili mbalimbali ambavyo vimeongezewa vipashio visivyohitajika. Hali hii inavifanya viambajengo vinavyohusika vikose sifa ya kuwa vya lugha ya Kiswahili kwa kuwa havileti maana au viwe tu na taarifa zisizohitajika wala kusaidia katika ubaini wa maana. Jambo hili linathibitishwa na data za uongezaji zinazooneshwa katika majedwali namba 6 hadi 8 ambapo sauti, silabi na vifungu vya maneno vimeongezwa.

Jedwali Na. 6: Makosa ya Uongezaji wa Sauti na Silabi katika KKK

Kidahizo	Fasili
cheichei	b. salamu inayotolewa kwa mtu mzima mwenye umri au rika linalofananana na yule anayeamkia; ambapo anayeamkiwa huitikia kwa kusema ‘cheichei’ (bwana/bibi).
fusi	udongo wa vumbi agh. unaotumika kutengenezea barababara za changarawe

ziara	b. mfulululizo wa michezo au maonyesho yanayofanywa na timu, au bendi ya muziki katika maeneo mbalimbali
--------------	---

Chanzo: BAKITA (2022)

Jedwali Na. 7: Makosa ya Uongezaji wa Sauti na Silabi katika KKF

Kidahizo	Fasili
mamachanja	lakabu anayoitumia agh. mume kumwita mkewe.
kumbukizi	<i>I.</i> sherehe ya kukumbuka mtu au tukilo la zamani.
koko²	kitendo cha kukusafisha pahali kwa kukumba au kukwangua takataka.

Chanzo: BAKIZA (2010)

Jedwali Na. 8: Makosa ya Uongezaji wa Kifungu cha Maneno katika KKS

Kidahizo	Fasili
ashiki²	tamaa ya kiume au kike ya kutaka kufanya mapenzi
batobato⁴	aina ya ugonjwa unaoshambulia mazao ya mizizi k.v. mihogo, viazi n.k.

Chanzo: TUKI (2019)

Data katika majedwali namba 6 na 7 zinaonesha uongezaji wa sauti na silabi usiohitajika. Katika Jedwali Na. 6, neno **linalofananana** katika kidahizo *cheichei* limeongezewa silabi **na** mwishoni. Neno sahihi lilipaswa kusomeka *linalofanana*. Uongezaji huu pia umejitokeza katika kidahizo *fusi*. Katika fasili ya *fusi*, kuna matumizi ya neno **barababara** ambalo limeongezewa silabi **ba** kati ya vijenzi **barabana-ra**. Neno kubalifu lilipaswa kusomeka *barabara*. Vilevile, kuna uongezaji wa silabi **i** mwanzoni mwa neno **ikinachotumika** wakati neno hilo haliihitaji silabi hiyo. Neno sahihi lilipaswa kusomeka *kinachotumika*. Katika Jedwali Na. 7, kitamkwa **-u-** kimeongezwa katika neno **kumwita**, katika kidahizo *mamachanja*. Neno sahihi lilipaswa kuwa *kumwita*. Kadhalika, kitamkwa **-l-** kimeongezwa katika neno **tukilo** katika kidahizo *kumbukizi*, ilhali neno sahihi lilipaswa kuwa *tukio*. Aidha, silabi **ku-** imeongezwa katika neno **kukusafisha** katika kidahizo *koko²* ambapo neno sahihi linapaswa liwe *kusafisha*. Nyongeza hii imefanyika pia katika KKS lakini yenyewe imevuka kiwango cha silabi na kujumuisha vifungu vya maneno. Katika Jedwali Na. 8, fasili ya kidahizo *ashiki²* imeongezwa kifungu cha maneno **ya kiume au kike** ambacho hakihitajiki. Hakukuwa na haja ya kueleza jinsi kwa sababu jinsi zote hupatwa na ashiki. Katika fasili ya kidahizo *batobato⁴*, kwenye jedwali hilo, kifungu cha maneno **aina ya** hakihitajiki kwa sababu hakimsaidii mtumia kamusi kuelewa maana ya batobato. Kilichopaswa kufanyika hapa ni kufafanua ugonjwa huo kwa uangavu, kwa mfano, ugonjwa unaoshambulia mazao ya mizizi k.v. mihogo na viazi na kufanya majani yake kuwa na mabaka au michirizi.

Suala la uongezaji vipashio si ugunduzi mpya kwa kuwa limejadiliwa pia na watafiti tangulizi. Kwa mfano, Ontieri (2022) aliyetumia istilahi ‘uchopekaji’, ameeleza uongezaji kuwa ni hali ambapo kipashio huongezwa katika neno, jambo linalosababisha kutokea kwa neno ambalo limesheheni vitamkwa vya ziada ambavyo havikupaswa kuwapo. Hali hii inapotokea, anahitimisha Ontieri, husababisha kutoeleweka kwa maana iliyokusudiwa. Kwa hiyo, matokeo ya utafiti huu yanazidi kuongeza maarifa katika yale yaliyopo kuhusiana na makosa ya kiuandishi. Waandishi wa kamusi wanahimizwa kuyaepuka ili kuhakikisha kwamba kamusi zao zinakuwa rafiki kwa watumiaji wanaowalenga.

4.3 Makosa ya Unafasishaji

Mdee (2010) anaeleza kuwa umbo la neno linaloingizwa katika kamusi ni lazima liwe lile ambalo mtumiaji wa kamusi anatarajiwa kulitafuta katika kamusi husika. Maelezo haya yanaendana na mtazamo wa Nadharia ya Urafiki wa Kamusi kwa Watumiaji. Kuhusiana na nafasi, Mdee anafafanua kwamba neno katika maandishi ni kipashio huria ambacho kwa kawaida huzungukwa na nafasi pande zote kinapoandikwa. Ikiwa uwekaji wa nafasi kati ya neno na neno hautazingatiwa, kuna hatari ya neno hilo kupoteza maana yake.

Utafiti huu umebaini kwamba changamoto ya kutozingatiwa kwa nafasi za maneno katika uandishi imejitokeza katika kamusi teule. Jambo hili limejitokeza kwa namna mbili. Kwanza, maneno zaidi ya moja yameandikwa pamoja bila kuacha nafasi. Pili, maneno ambatani yameandikwa kwa kutengwa na nafasi kinyume na utaratibu unaokubalika. Makosa ya namna hii yanabainishwa kwa wino uliokoza katika fasili za vidahizo zilizooneshwa kwenye majedwali namba 9 hadi 11.

Jedwali Na. 9: Makosa ya Unafasishaji wa Maneno katika KKK

Kidahizo	Fasili
topetope ¹	aina ya tunda ambalo ganda lake lina vinundunundu kama stafeli na ambalo ndani lina nyama nyeupe na mbegu nyeusi linalotokana nammea wa mtopetope

Chanzo: BAKITA (2022)

Jedwali Na. 10: Makosa ya Unafasishaji katika KKF

Kidahizo	Fasili
agana ²	kitendo cha watu kuambiana kwaheri .
alamsiki!	tamko la kuagana; kwaheri .

Chanzo: BAKIZA (2010)

Jedwali Na. 11: Makosa ya Uunganishaji wa Maneno katika KKS

Kidahizo	Fasili
aga	omba ruhusa ya kuondoka; sema kwaheri

Chanzo: TUKI (2013)

Majedwali namba 9 hadi 11 yanaonesha namna makosa ya unafasishaji wa maneno yalivyojitokeza katika fasili za vidahizo vya kamusi teule. Tukianza na KKK, Jedwali Na. 9 linaonesha kwamba fasili ya kidahizo *topetope*¹ ina maneno mawili, **na** na **mmea**, ambayo yameunganishwa na kuwa neno moja **nammea** lisilo na maana yoyote katika lugha ya Kiswahili. Muunganiko huu ulipaswa utenganishwe ili vijenzi vyake visimame kama maneno mawili tofauti yanayojitegemea. Neno la kwanza ni **na** (kiunganishi) na la pili ni **mmea** (nomino). Hivyo, ilipaswa yatenganishwe na kuwa ...**na mmea**.... Aidha, kosa la uunganishaji maneno tunaliona pia katika Jedwali Na. 10 na Jedwali Na. 11 ambapo neno **kwaheri** katika fasili za vidahizo *agana*² na *aga* kutoka KKF na KKS mtawalia yameunganishwa badala ya kuandikwa kwa usahihi kwa kutenganisha kihusishi **kwa** na nomino **heri** na kutupatia kirai kihusishi *kwa heri*. Maneno hayohayo tena yanajitokeza yakiwa yameunganishwa hivyo hivyo katika kidahizo *alamsiki* katika KKF. Kwa kawaida, mtazamo huu unaweza kusailiwa na wasomaji wa makala haya kwa sababu kirai hicho kimekuwa kikiandikwa kimakosa kwa mazoea. Muundo wa kirai hicho, ambacho kimeoneshwa kimakosa kama neno moja, hauna tofauti na wa viungo vya ushikamani kama vile ‘kwa sababu’ na ‘kwa minajili’.

Namna nyingine ya kosa la unafasishaji inayojitokeza katika KKK na KKF, ambayo haikuonekana katika KKS, ni kuacha nafasi au kuongeza kistari katika neno ambatani au neno radidi linalopaswa kuandikwa bila nafasi wala kistari baina ya maneno yanayoliunda. Jambo hili litokeapo, husababisha neno husika kuonekana kama uradidi au kama maneno mawili tofauti. Maneno yaliyopatikana na shida hii katika data ni **kufa-fanua** katika kidahizo *zebe*, **kuto-kana** katika kidahizo *a!* (KKK) na **mbali mbali** katika kidahizo *balbu* (KKF).

Katamba (2006) anafafanua kuhusu miundo ya maneno ambatani. Kiothografia, kuna maumbo ambatani yaliyounganishwa, yasiyounganishwa na maumbo yenye kistari. Hivyo, kila neno ambatani lina muundo na namna yake ya kuandikwa. Utaratibu unaoelezwa na Katamba haukuzingatiwa katika data zilizotolewa katika utafiti huu, jambo ambalo linaonesha kwamba yaliyofanyika ni makosa yanayozikoshesha kamusi teule urafiki kwa mtumiaji na, hivyo, kumwathiri mtumiaji kwa kumkosesha maana iliyokusudiwa au kwa kumkera. Lupogo (2020) na Stephano (2023) wanayajadili kwa kina makosa ya unafasishaji wakitumia istilahi za “makosa ya uunganishaji” na

“makosa ya utenganishaji”. Stephano (2023) anabainisha kwamba makosa ya aina hii yanatabirika. Hata hivyo, makosa yanayotabirika yanahusu maneno yenye urejeshi, maneno yenye kiambishi cha umahali na wakati, maneno yanayotokana na uradidi, na maneno ambatani kwa upande wa utenganishaji na mwambatano wa vitenzi shirikishi vya “kuwa na” na nomino, na viunganishi tegemezi vinavyoanza na “kwa” kwa upande wa utenganishaji, ambayo hayadhahiriki katika data yetu.

4.4 Makosa ya Kubadili Mpangilio wa Viambajengo katika Tungo

Data zinaonesha kuwapo kwa tungo (maneno, virai, vishazi na sentensi) zilizotumika katika fasili za vidahizo ambazo mpangilio wa viambajengo vyake si sahihi, jambo lililosababisha tungo husika ama kutokuwa sehemu ya msamiati au kukosa usarufi wa lugha ya Kiswahili au, pengine, kuleta tu uvulivuli katika maana. Hali hii inaleta changamoto kwa msomaji kuelewa kirahisi maana iliyomo katika fasili husika. Baadhi ya tungo za ngazi ya neno ambazo mpangilio wa viambajengo vyake umechanganywa zinabainishwa katika Jedwali Na. 12 na zile za ngazi ya kirai zinabainishwa katika Jedwali Na.13.

Jedwali Na. 12: Makosa ya Mpangilio wa Viambajengo katika KKK

Kidahizo	Fasili
lao	kivumishi kimikilishi cha ngeli ya li-/ya- nafsi ya tatu wingi
nusukipenyo	b. umbali kutoka katikati ya duara kwenda sehemu yoyote ya uso wa daura

Chanzo: BAKITA (2022)

Jedwali Na. 13: Makosa ya Mpangilio wa Viambajengo katika KKS

Kidahizo	Fasili
akserereta	kifaa maalumu katika gari cha kuongezea kasi
kaki ²	kitambaa cha pamba kizito

Chanzo: TUKI (2019)

Majedwali namba 12 na 13 yanaonesha makosa ya mpangilio wa viambajengo. Katika fasili ya kidahizo *lao*, kuna uchanganyaji wa silabi katika neno **kimikilishi**. Katika neno hili, silabi **-li-** ilipaswa ifuate baada ya **kimi-**, silabi **-ki-** ikifuatiwa na silabi **-shi** mwishoni ili kupata neno sahihi *kimilikishi*. Vilevile, neno **daura** lililopo katika kidahizo *nusukipenyo* lina makosa ya kuchanganya vitamkwa. Katika neno hili, kitamkwa **-u-** kilipaswa kufuata baada ya kitamkwa **d-** na kisha kufuatiwa na kitamkwa **-a-** kabla ya **-ra** mwishoni ili kupata neno sahihi *duara*.

Katika Jedwali Na. 13, kipashio **kifaa maalumu**, katika fasili ya *akserereta*, kilipaswa kufuatwa na kipashio **cha kuongezea kasi** ambacho ni kikumushi chake. Kwa pamoja, vipashio hivi vilipaswa kuunda kiambajengo **kifaa maalumu cha kuongezea kasi**

ambacho kingefuatwa na kipashio **katika gari**. Hata hivyo, waandishi walichanganya vipashio hivi kwa kuchomeka kipashio **katika gari** katikati ya tungo na hivyo kukifanya kisiwe na sarufi sahihi. Kadhalika, jambo hili tunalionga katika fasili ya kidahizo *kaki*² ambapo kipashio **cha pamba** kimechopekwa katikati ya kipashio **kitambaa kizito** ambacho kimetenganishwa na uchopekaji huo.

Ontieri (2022) anafafanua kuhusu makosa ya mpangilio wa viambajengo akijielekeza katika kamusi. Hulusani, yeye anajielekeza katika ngazi ya neno tu. Anaeleza kuwa kosa hili hutokana na matumizi ya fonimu fulani mahali ambapo fonimu sahihi ilipaswa kuwapo. Jambo hili hufanya neno husika kutokuwa la Kiswahili na, hivyo, maana na ujumbe wake huweza kupotea, hali inayowaathiri watumiaji kwa kukosa maana lengwa au kukerwa na uandishi.

4.5 Makosa ya Uteuzi wa Maneno/Msamiati

Utafiti huu umebaini kuwa kuna makosa ya uteuzi wa maneno yaliyotumika katika fasili za vidahizo vya kamusi teule. Maneno yasiyo mwafaka yametumika, jambo linalowasababishia watumiaji ugumu wa kuelewa maana ya kidahizo husika. Maneno hayo ni sahihi na kubalifu katika lugha ya Kiswahili, lakini yametumika mahali pasipo pake kama data za majedwali namba 14 hadi 16 zinavyoonesha.

Jedwali Na. 14: Makosa ya Uteuzi wa Maneno katika KKK

Kidahizo	Fasili
kimbio	hali ya kukukimbia ; kwenda kwa kasi
tupia	<i>a.</i> weka kanga ua mtandio begani au kichwani
sema	<i>ch.</i> zungumzia habari za mtu kwa usiri bila ya yeye mwenye kuwapo au kusikia

Chanzo: BAKITA (2022)

Jedwali Na. 15: Makosa ya Uteuzi wa Maneno katika KKF

Kidahizo	Fasili
dasturi ²	<i>l.</i> kipande cha mti kinachofungwa mbele ua jahazi, dau au mashua ili kizuie kamba ya joshi wakati wa kutweka.
kinywa	sehemu iliyo wazi katika mwilini agh. kichwani unaotumiwa na kiumbe hai kulia au kunywea; = mdomo.

Chanzo: BAKIZA (2010)

Jedwali Na. 16: Makosa ya Uteuzi wa Maneno katika KKS

Kidahizo	Fasili
kaukiana	2 konda sana kwa mtu 3 (ms) askari wamesimama katika hali ya ukakamavu
abee!	neni la kuitikia mtu, hasa mwanamke
angalau	neni litumikalo kueleza jambo lililo bora zaidi
usambazaji	hali ya kueneza vitu au huduma k.v. maji, umeme au mawasiliano

Chanzo: TUKI (2019)

Katika Jedwali Na. 14, neno **kukukimbia** limeteuliwa katika fasili ya *kimbio*. Hata hivyo, neno hili si mwafaka katika muktadha huu ambapo neno *kukimbia* lilipaswa kutumika. Kadhalika, neno **au** lilipaswa kutumika badala ya neno **ua** katika fasili ya kidahizo *tupia*. Vilevile, katika fasili ya kidahizo *sema*, kuna matumizi ya neno **mwenye** mahali ambapo palipaswa kuwa na neno **mwenyewe**. Makosa ya namna hii pia yanaonekana katika Jedwali Na. 15 ambalo linaonesha mifano ya maneno yaliyotumika kimakosa katika fasili za vidahizo vya KKF. Katika kidahizo *dasturi*², neno **ua** limetumika mahali palipopaswa kuwa na neno **ya**. Aidha, neno **mwilini** katika kidahizo *kinywa* limetumika visivyo badala ya neno **mwili**.

Tofauti na uteuzi usio sahihi wa neno mojamoja katika KKK na KKF, katika KKS kuna vifungu vya maneno vilivyoteuliwa visivyo. Mathalani, data ya Jedwali Na. 16 inaonesha kuwa katika fahiwa ya pili ya kidahizo *kaukiana*, kifungu cha maneno **kwa mtu** kimezimishwa kuwekwa mahali ambapo hakihitajiki kabisa kwa kuwa hata kikiondolewa, maana iliyokusudiwa inapatikana. Aidha, katika fahiwa ya tatu ya neno hilohilo, kifungu **katika hali ya** kimetumika kimakosa badala ya neno moja **kwa**. Mbali na uteuzi usio sahihi wa vifungu vya maneno, data ya Jedwali Na. 16 pia inaonesha uteuzi usio mwafaka wa neno mojamoja. Kwa mfano, matumizi ya neno **hali** katika fasili ya kidahizo *usambazaji* si mwafaka kwani mahali pa neno hilo palipaswa kuwa na neno **tendo** au **kitendo**. Kadhalika, matumizi ya neno **hasa** katika fasili ya kidahizo *abee!* yanaonesha kuwa, mbali na mwanamke, mwanamume pia anaweza kuitika abee, jambo ambalo si la kweli. Hivyo, neno mwafaka hapa lilipaswa kuwa **hususani** au pengine linahitaji kuondolewa kabisa na kuwa tu na fasili kama “neni linalotumiwa na mwanamke kuitikia”.

Suala la matatizo ya uteuzi wa msamiati mwafaka katika matini si jambo jipya kwa kuwa limejadiliwa pia na watafiti tangulizi. Mathalani, katika utafiti wake kuhusu makosa hayo katika vyombo vya habari, King`ei (2000) anaeleza kuwa makosa ya uteuzi wa msamiati hujitokeza na hutokana na kiwango duni cha ujuzi wa msamiati miongoni mwa waandishi wa habari. Hivyo, anasisitiza kuwa mwandishi mzuri

anapaswa awe na uwezo wa kumudu ipasavyo msamiati unaostahili kutumika katika nyanja mbalimbali. Kwa hiyo, utafiti huu unaongeza maarifa katika yale yaliyopo na kusisitiza kwamba makosa ya uteuzi wa msamiati yamekuwa tatizo sugu linalojirudiarudia hata katika maandiko nyeti na, hivyo, linahitaji umakini kwa waandishi kuachana na makosa ya aina hii.

4.6 Makosa ya Matumizi ya Njeo

Data tulizozipata kutoka kamusi teule zinaonesha matumizi mabaya ya nyakati katika baadhi ya vitenzi vilivyotumika katika fasili za vidahizo, jambo linalofanya fasili husika kutowasilisha vyema maana iliyokusudiwa. Makosa hayo yamejitokeza katika KKK pekee kama inavyobainishwa katika Jedwali Na. 17.

Jedwali Na. 17: Makosa ya Matumizi ya Njeo katika KKK

Kidahizo	Fasili
kashda	kitambaa chepesi kilinachovaliwa begani agh. na wanaume wa Kiislamu, mashehe

Chanzo: BAKITA (2022)

Katika Jedwali Na. 17, data inaonesha kuwa kuna matumizi mabaya ya nyakati. Mathalani, katika fasili ya kidahizo *kashda*, kuna matumizi ya nyakati mbili katika kitenzi kimoja. Kwa hiyo, mbali na kuwa kosa la matumizi ya njeo, hili pia linaweza kuwa kosa la uongezaji. Katika kitenzi **kilinachovaliwa**, kuna viambishi awali vya njeo mbili tofauti: wakati uliopita na wakati uliopo, hali endelevu. Kiambishi awali **-li-** kinaonesha njeo ya wakati uliopita na kiambishi awali **-na-** kinaonesha hali endelevu ya njeo ya wakati uliopo. Matumizi ya nyakati mbili katika kitenzi kimoja yanaondoa mantiki na uelewekaji wa maana na, hivyo, kuwakanganya watumiaji wa kamusi lengwa. Katika muktadha huu, njeo ya wakati uliopo, hali endelevu, ndiyo ingetumiwa peke yake badala ya kuambatanishwa na njeo ya wakati uliopita.

Suala la matatizo ya matumizi yasiyo sahihi ya njeo si jambo geni kwani limefafanuliwa pia na Obara (2014). Obara anaeleza kuwa njeo hueleza uhusiano uliopo kati ya wakati wa kutamka na wa kutenda jambo. Anaendelea kueleza kuwa waandishi wengi hutatizika wanapotumia njeo na hali katika kazi zao. Hivyo, huchanganya viambishi njeo kiasi kwamba wakati uliokusudiwa haubainiki wazi. Jambo hili huleta utata wa kuelewa maana iliyokusudiwa kama ilivyobainika katika data ya Jedwali Na. 17.

4.7 Makosa ya Matumizi ya Herufi Kubwa na Ndogo

Herufi kubwa hutokea mwanzoni mwa sentensi, majina ya watu na mahali (BAKITA, 2013). Katika uandishi, ni kawaida kwa mwandishi kuchanganya herufi kubwa na ndogo katika matini mbalimbali. Hata hivyo, licha ya herufi ndogo kutawala, herufi kubwa pia hutumika. Herufi kubwa, mara nyingi, hutumika katika kuanzisha sentensi, mwanzoni mwa nomino za kipekee, kuonesha kichwa au mada na kuonesha maneno yaliyofupishwa. Matumizi hayo ya herufi kubwa na ndogo yanaonekana kuwa na changamoto katika KKK na KKF kama inavyobainishwa katika data za majedwali namba 18 na 19.

Jedwali Na. 18: Makosa ya Matumizi ya Herufi Kubwa na Ndogo katika KKK

Kidahizo	Fasili
Ki wolfu	lugha ya kiafrika iliyokuwa na hati zake yenyewe inayotumika (Afrika Magharibi)
shali	a. kitambaa kizito ambacho huvaliwa mabegani na viongozi wa dini ya kiislamu au watu wa makamu; kashida
fasiki	mtu mwenye tabia ya kuzini kis.: asherati, mzinzi, mzinifu, mkware, Malaya , mtalaleshi, guberi

Chanzo: BAKITA (2022)

Jedwali Na. 19: Makosa ya Matumizi ya Herufi Kubwa na Ndogo katika KKF

Kidahizo	Fasili
kiumbe	vitu kama mtu, ndege, mnyama, miti ambavyo hupewa uhai na mwenyezi Mungu .

Chanzo: BAKIZA (2010)

Majina yaliyokoza wino katika fasili za vidahizo kwenye majedwali namba 18 na 19 ni ya pekee, isipokuwa **Malaya**. Kwa kawaida, majina ya aina hiyo hupaswa kuanza kwa herufi kubwa popote yanapojitokeza. Hata hivyo, hali ni tofauti katika data hii. Neno **mwenyezi** katika kidahizo *kiumbe* limeanza kwa herufi ndogo badala ya herufi kubwa na kuwa **Mwenyezi Mungu**. Aidha, neno **kiafrika** lilipaswa kuandikwa **Kiafrika** katika fasili ya *Ki wolfu*. Kwa upande mwingine, majina ya kawaida huanza kwa herufi ndogo. Hali hii ni tofauti katika kidahizo *fasiki* ambapo neno **Malaya** lilipaswa kuwa **malaya**.

Suala la matumizi sahihi ya herufi kubwa limefafanuliwa pia na BAKITA (2013) ambalo linaeleza kuwa herufi kubwa hutumika wakati wa kuandika herufi ya kwanza katika sentensi, baada ya alama ya nukta, kiulizo, mshangao na baada ya alama za mnukuo. Pia, inafafanuliwa kuwa herufi kubwa hutumika wakati wa kuandika herufi ya kwanza ya majina ya kipekee. Hivyo, ni muhimu kwa mwandishi wa matini yoyote

kuzingatia matumizi sahihi ya herufi kubwa na ndogo katika matini. Jambo hili lisipofanywa, humwonesha mwandishi kuwa ni mtu asiye makini na kazi yake na hivyo huwakera wasomaji. Kwa sababu hiyo, matini isiyozingatia matumizi sahihi ya herufi kubwa hukosa hali ya urafiki kwa msomaji wake.

4.8 Makosa ya Uakifishaji

Uakifishaji ni utumiaji wa alama za uandishi ili kuyawezesha maandishi kueleweka vizuri kwa wasomaji. Uakifishi huhusisha uwekaji wa alama za mkato (.), nukta (.), nuktamkato (:), nuktapacha (:), kiulizo (?), mabano ((), {}, []), wimbi (~), mshangao (!), ritifaa (^), mkwaju (/) na alama za kufungua na kufunga usemi kwa lengo lililotajwa (BAKITA, 2022). Uzingatiaji wa matumizi sahihi ya alama hizi husaidia katika uelewekaji wa maana inayokusudiwa kuwasilishwa katika matini husika. Akifafanua kuhusu umuhimu wa uakifishaji, King`ei (2014) anasema kuwa lengo la uakifishaji ni kuhakikisha kwamba maandishi yana udhahiri au uwazi na usomekaji. Katika kamusi teule, kuna ukiukaji wa matumizi ya alama hizi kwa kiasi fulani. Data katika majedwali namba 20 na 21 zinadhihirisha ukiukaji wa matumizi ya alama hizo.

Jedwali Na. 20: Makosa ya Matumizi ya Alama za Uakifishaji katika KKK

Kidahizo	Fasili
mdanzi	mmea unaofanana na mchu-ngwa unaozaa matunda makubwa yenye ganda nene na ladha kali kuliko machungwa
a!	<i>b.</i> tamko linaloashiria maumivu apatayo mtu kuto-kana na kuumwa, kung`atwa au kuchomwa na kitu
adibisha	fanya mtu awe na adabu; tia mtu adabu <i>kiny.:</i> <i>potosha = adibishia, adibishika, adibishwa, adibi-shana</i>
zebe	mtu asiyeitumia akili yake ipasavyo au asiye na uwezo wa kufa-fanua na kutathmini jambo
Kiwolfu	lughu ya kiafrika iliyokuwa na hati zake yenyewe inayotumika (Afrika Magharibi)

Chanzo: BAKITA (2022)

Jedwali Na. 21: Makosa ya Matumizi ya Alama za Uakifishaji katika KKF

Kidahizo	Fasili
fawidhi	1 kitendo cha mtu kumpa dhamana mwengine amtunzie kitu chake./ kitendo cha mtu kumpa mtu mwengine kitu ili akihifadhi.
kambare	samaki wa maji baridi mwenye umbo la mviringo kichwa na rangi nyeusi-nyeusi .

Chanzo: BAKIZA (2010)

Majedwali namba 20 na 21 yanaonesha jinsi alama za uakifishaji zilivyotumika kimakosa. Katika Jedwali Na. 20, fasili za vidahizo *mdanzi, a!*, *adibisha* na *zebe* zina alama ya kistari (-) iliyotumika mahali pasipostahili kwenye maneno **mchu-ngwa**, **kuto-kana**, **adibi-shana** na **kufa-fanua** mtawalia. Maneno haya huandikwa bila kuwa na kistari chochote; yaani, mchungwa, kutokana, adibishana na kufafanua. Katika jedwali hilohilo, kwenye fasili ya kidahizo *Kiwolfu*, mabano yametumika visivyo kwa sababu maneno yaliyofungiwa kwenye mabano hayakupaswa kufungiwa. Jedwali Na. 21 pia linadhihirisha kuwapo kwa kosa la kiuakifishaji. Katika kidahizo *fawidhi*, baada ya neno **chake**, pana **nukta** ambayo ilipaswa iwe mwishoni mwa fasili. Aidha, baada ya neno **chake**, kuna matumizi ya alama ya **nukta** (.) pamoja na mkwaju (/). Vilevile, katika kidahizo *kambare*, neno ambatani **nyeusi-nyeusi** limeandikwa kwa kuwekewa kistari katikati, jambo ambalo si sahihi kwani neno hilo linapaswa kuandikwa pasipo kuwekwa kistari, yaani *nyeusinyeusi*. Makosa haya yanazikoshesha kamusi teule hali ya kuwa rafiki kwa mtumiaji.

Suala la matumizi ya alama za uakifishaji, mathalani, alama ya kistari, limejadiliwa na BAKITA (2013) ambapo inafafanuliwa kuwa alama ya kistari hutumika ili kutenganisha maelezo ya nyongeza na yale ya msingi; hutumiwa badala ya nuktapacha kutenganisha mzungumzaji na maelezo yake; hutumika kuonesha jina la mwandishi au msemaji ambaye usemi au dondoo lake limekaririwa n.k. Matumizi ya kistari katika data za Jedwali Na. 20 na Jedwali Na. 21 yanakinzana na ufafanuzi huu na, hivyo, kuthibitisha kuwa ni makosa. Makosa ya kiuakifishi yameshughulikiwa kwa kina na Stephano (2018) ambaye anaonesha kuwa ni matokeo ya kwenda kinyume na Nadharia Tumizi ya Uakifishaji, na Lupogo (2020) ambaye amebainisha mifano mbalimbali na kuhitimisha kuwa ni miongoni mwa makosa yaliyozoeleka. Hata hivyo, tafiti hizi tangulizi hazikuangazia kamusi.

4.9 Makosa ya Upatanisho wa Kisarufi na ya Kimantiki

Upatanisho wa kisarufi ni kukubaliana kisarufi kunakojitokeza kati ya nomino kiima na kitenzi au kivumishi kunakobainishwa na viambishi (BAKITA, 2022). Kukosekana kwa upatanisho wa kisarufi huondoa mantiki pamoja na maana iliyokusudiwa. Data zilizokusanywa katika utafiti huu zinaonesha kuwa kuna makosa ya upatanisho wa kisarufi katika baadhi ya fasili za vidahizo vya kamusi teule kama inavyodhihirishwa na data za majedwali namba 22-24.

Jedwali Na. 22: Makosa ya Upatanisho wa Kisarufi katika KKK

Kidahizo	Fasili
kitanga ³	kibakuli cha mizani kinachowekeka vitu ili kupima uzito chake
banjua	a. pasua mti na kuufanya mbao mfano wa vibanzi ya kujengea ghala.

Chanzo: BAKITA (2022)

Jedwali Na. 23: Makosa ya Upatanisho wa Kisarufi katika KKF

Kidahizo	Fasili
kindumbwendumbwe ¹	nyimbo inayoimbwa kumfanyia tashtiti mtoto mwenye tabia ya kukojoa kitandani.
chungu ³	upele vidogovidogo visivyosikamana; = pele.
kinywa	sehemu iliyo wazi katika mwilini agh. kichwani unaotumiwa na kiumbe hai kulia au kunywea; = mdomo.

Chanzo: BAKIZA (2010)

Jedwali Na. 24: Makosa ya Upatanisho wa Kisarufi na ya Kimantiki katika KKS

Kidahizo	Fasili
afezia	ukosefu wa uwezo wa kusema au kuelewa lugha kunakosababishwa na kuumia ubongo
kayamba	tuwazi ambayo hutengenezwa kwa matete na ndani likatiwa punje kavu au changarawe na kutikiswa linapopigwa wakati wa ngoma au wa kuimba
Afro	Mtindo wa kuacha nywele, hasa za kipilipili ziwe nyingi

Chanzo: TUKI (2019)

Majedwali Na. 22-24 yanaonesha data zinazodhihirisha kujitokeza kwa makosa ya upatanisho wa kisarufi na ya kimantiki katika fasili za vidahizo vya kamusi teule. Katika KKK (Jedwali Na. 22), sehemu ya fasili ya kidahizo *kitanga*³ iliyokoza wino ...**uzito chake** haioneshi upatanisho wa kisarufi baina ya neno **uzito** na **chake**. Neno **wake** lingeweza kutumika na kuwa ...**uzito wake** na kuleta maana iliyokusudiwa. Vilevile, jambo hili linajitokeza katika fasili ya kidahizo *banjua* ambapo kihusishi **ya** kimetumika badala ya **vya**. Hivyo, badala ya vibanzi kupatanishwa na kihusishi **ya** (...**vibanzi ya kujengea**...), vilipaswa kupatanishwa na **vya** na kuwa ...**vibanzi vya kujengea**....

Kadhhalika, katika KKF (Jedwali Na. 23), kumbainika kuwapo kwa makosa ya upatanisho wa kisarufi, hali inayosababisha kutoweka kwa mantiki. Mithalani, katika kidahizo *kindumbwendumbwe*¹, kuna kifungu cha maneno “**nyimbo inayoimbwa**...” ambacho hakina upatanisho kwa kuwa neno **nyimbo** ama liko katika wingi au ngeli ya n/n lakini kitenzi **inayoimbwa** ama kiko katika umoja au ngeli tofauti. Utungo huu ulipaswa kusomeka “*nyimbo zinazoimbwa* ...” au “*wimbo unaoimbwa*...” Pia, katika

fasili ya kidahizo *chungu*³, kuna kifungu cha maneno “**upele vidogvidogo...**” badala ya kuwa “**upele mdogomdogo...**” au “**vipele vigogvidogo...**” Na katika fasili ya kidahizo *kinywa*, hakuna upatanisho baina ya neno kuu ‘**sehemu**’ na kitenzi ‘**unaotumiwa**’. Fasili hiyo ilipaswa kusomeka, “Sehemu iliyo wazi katika mwili agh. kichwani **inayotumiwa** na kiumbe hai kulia au kunywea”.

Katika KKS (Jedwali Na. 24), makosa ya upatanisho wa kisarufi na ya kimantiki yamebainika pia. Mathalani, neno **ukosefu**, katika fasili ya kidahizo *afezia*, halipatani na kitenzi **kunakosababishwa** ambacho kinalifafanua. Jambo hili linatokana na kutofautiana kwa ngeli; neno **ukosefu** likiwa katika ngeli ya u/u ilhali **kunakosababishwa** likiwa katika ngeli ya **ku**. Vivyo hivyo, neno **tuwazi** katika fasili ya kidahizo *kayamba* halieleweki lipo katika ngeli gani kwa kuwa urejeshi wake (**ambayo**) upo katika ngeli ya n/n, lakini vitenzi (**likatiwa** na **linapopigwa**) vinarejelea ngeli ya **ji-/ma-**. Kadhalika, katika fasili ya kidahizo *Afro*, kuna kifungu cha maneno ‘**ziwe nyingi**’ ambacho kinapotosha maana. Hii ni kwa sababu, nywele zinapoachwa kufanya mtindo wa Afro, hazifanywi kuwa nyingi bali lengo ni kuziacha ziwe ndefu.

Makosa ya upatanisho wa kisarufi si mageni kwa kuwa yameshajadiliwa na tafiti zingine zilizotangulia. Mathalani, Obara (2014) anaeleza kwamba makosa ya upatanisho wa kisarufi hutokana na ukiushi wa viambishi vipatanishi vya ngeli. Mwandishi anapoteua kiambishi kisicho mwafaka katika tungo anakuwa amefanya kosa la kisarufi. Hivyo, uandishi bora ni ule unaozingatia kanuni za kisarufi za lugha kwa kuteua viambishi faafu ili kuleta maana iliyokusudiwa. Kwa sababu hiyo, kamusi, kama maandiko yanayoaminiwa sana na watumiaji wa lugha, zinapaswa kuliepuka tatizo hili. Kuendelea kuwa na makosa ya namna hiyo kunazifanya kamusi zikose kuwa rafiki kwa mtumiaji.

5.0 Hitimisho

Lengo la makala haya si kubeza kazi nzuri iliyofanywa katika kamusi teule. Tunatambua kuwa kamusi hizo ni bora na zimesheneni msamiati wa kutosha pamoja na mifano ya matumizi yenye kuendana na miktadha mbalimbali. Hakika, wengi tunanufaika kwa kuwapo kwa kamusi hizo. Hata hivyo, tunaona kwamba ubora wa kamusi hizi unaweza kuongezwa zaidi kwa kuziepuka changamoto kadhaa za kiuandishi ambazo zimebainishwa katika makala haya kwani zina madhara kwa kamusi yenyewe, kwa watumiaji na kwa maendeleo ya Kiswahili kwa kuwa zinazikoshesha kamusi teule sifa ya kuwa rafiki kwa mtumiaji. Kwa hiyo, kupitia makala haya ambayo yamebainisha makosa ya kiuandishi, pamoja na athari zake, waandaaji wa kamusi husika wanaweza kurekebisha makosa hayo ili matoleo yajayo yawe bora zaidi.

Marelejeo

- BAKITA (2013) *Mwongozo kwa Waandishi wa Kiswahili Sanifu* (Toleo la Pili). Dar es Salaam: TUKI.
- BAKITA (2022) *Kamusi Kuu ya Kiswahili* (Toleo la Pili). Nairobi: Longhorn Publishers Ltd.
- Chuwa, A. R. (2004) "Problems in Swahili Lexicography". *Lexikos*. Juz. 6: 323-329.
- Genc, B., Mavasoglu, M. na Bada, E. (2010) "Types and Functions of Repetitions in the Narrations of Turkish Speakers of French". *Novitas-ROYAL*, Juz. 4(2): 216-224.
- Hans, M. M. (2012) "*Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (2004): Changamoto na Namna ya Kukabilia Nazo". *Kiswahili*, Juz. Na. 75: 52-63.
- Hartmann, R. R. K. (1983) "The Bilingual Learner's Dictionary and Its Users". *Multilingua*, Juz. Na. 2(4): 195-200.
- Hartmann, R. R. K. (2001) *Teaching and Researching Lexicography*. Harlow: Pearson Education.
- Jackson, H. (2002) *Lexicography: An Introduction*. London: Routledge.
- King`ei, K. (2000) "Matatizo ya Matumizi ya Lugha katika Vyombo vya Habari: Mifano kutoka Kenya". *Swahili Forum*, Juz. Na. 7: 45-56.
- King`ei, K. (2014). *Taaluma ya Uandishi*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.
- Kombo, D. K. na Tromp, D. L. (2006) *Proposal and Thesis Writing: An Introduction*. Nairobi: Pauline Publications Africa.
- Lupogo, I. (2020) "Kukithiri kwa Makosa Yaliyozoeleka katika Matumizi ya Kiswahili Sanifu: Uchunguzi wa Makosa Maalumu. *Jarida la CHALUFAKITA*, Juz. Na. 2: 1-17.
- Matinde, R. S. (2012). *Dafina ya Lugha: Isimu na Nadharia, kwa Sekondari, Vyuvo vya Kati na Vyuvo Vikuu*. Mwanza: Serengeti Educational Publishers (T) Ltd.
- Mdee, J. S. (2004) "Kirkeby's *English-Swahili Dictionary*". *Lexikos*, Juz. Na. 14: 369-395.
- Mdee, J. S. (2010). *Nadharia na Historia ya Leksikografia*. Dar es Salaam: TUKI.
- Mnenuka, A. (2010) "Dhima ya Uradidi katika Mawasiliano ya Kiswahili: Uimarishaji na Udhoofishaji wa Maana". *Kiswahili*, Juz. Na. 73(1): 32-44.
- Mwenda, M. (2016) "Tahakiki ya Kamusi ya Maana na Matumizi". *Mara Research Journal of Kiswahili*, Juz. Na. 1: 51- 60.
- Obara, J. M. (2014). Uchanganuzi wa Makosa Yanayofanywa na Wanafunzi Wazungumzaji wa Lugha ya Ekegusii. Tasnifu ya Shahada ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Ontieri, J. O. (2022) "Athari za Kifonolojia za Lugha ya Kwanza katika Kiswahili: Mfano wa Lugha Teule za Kibantu Nchini Kenya". *Mulika*, Juz. Na. 34: 1-13.

- Rubanza, Y. I. (1996) *Mofolojia ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Rubanza, Y. I. (2006) Vidokezo vya Mofolojia ya Kitenzi katika Luzinza. *Kioo cha lugha*, Juz. Na. 4(1): 62-71.
- Stephano, R.O. (2018) “Ukiukwaji wa Nadharia Tumizi ya Uakifishaji katika Kazi za Kitaaluma za Wanafunzi wa Shule za Msingi Tanzania”. *Mulika*, Juz. Na. 37: 151-168.
- Stephano, R.O. (2023) “Utabirifu wa Makosa ya Utenganishaji na Uunganishaji wa Maneno katika Kiswahili”. *Mulika*, Juz. Na. 42 (2): 184-196.
- TUKI (2013) *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (Toleo la Tatu). Nairobi: Oxford University Press.
- Wanyenya, W. (2015) “Makosa Yanayofanywa na Wanafunzi Wanaojifunza Kiswahili kama Lugha ya Pili katika Shule za Sekondari Nchini Uganda”. *Kiswahili*, Juz. Na. 78(1): 115-22.
- Wiegand, H. E. (1983) “On the Structure and Contents of a General Theory of Lexicography”. Katika Hartmann, R. (Mh.) *LEXeter '83 Proceedings: Papers from the International Conference on Lexicography at Exeter, 9–12 September 1983* (kur. 13-30). Berlin, Boston: Max Niemeyer Verlag. <https://doi.org/10.1515/9783111593166-005>.